



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI
TAARIFA KWA VYOMBO VYA
HABARI



UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA

MKOANI DAR ES SALAAM

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa Mkoa wa Dar es salaam kuwa itaendesha zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kutumia teknolojia ya "Biometric Voters Registration (**BVR**) kuanzia tarehe **22/07/2015** hadi **31/07/2015**.

Vituo vya Uandikishaji vitakuwa kwenye Mitaa.

Watakaohusika katika zoezi hili ni wananchi wote:-

- Waliotimiza umri wa **Miaka 18** na watakaotimiza **Miaka 18** ifikapo mwezi **Oktoba 2015**.
- Waliojiandikisha awali kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili kuhuisha taarifa zao na kupata kadi mpya za kupigia kura.
- Wote ambao wanazo sifa lakini hawajawahi kujiandikisha

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawakumbusha wale wote walio na kadi za zamani kwenda nazo kituoni. **Aidha wale wote waliojiandikisha wakati wa zoezi la Majaribio katika kata za Bunju na Mbweni Wilayani Kinondoni watatakiwa kufika vituoni wakiwa na kadi hizo ili kurahisisha uhamishaji wa taarifa zao kwenye mfumo mpya wa utambuzi wa Wapiga Kura.**

Tume inapenda kuwakumbusha Wananchi umuhimu wa kujiandikisha kwenye vituo vilivyo kwenye maeneo yao ambako ndiko watakakopigia Kura siku ya Uchaguzi Mkuu Oktoba 25, 2015 Tume inawatahadharisha wananchi kutojaribu kujiandikisha zaidi ya mara moja kwani mashine zitawatambua na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao .Pia inawatahadharisha wale wasio Raia wasijaribu kujiandikisha katika Daftari la Wapiga Kura kwani ni kosa la jinai.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapenda kuwasisitiza wananchi wote wa Dar es Salaam kujitokeza kwa wingi ili waweze kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwani ndiyo hatua muhimu ya kuwawezesha kupigia Kura na kuchagua viongozi wao.

Tangazo hili limetolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, S.L.P. 10923, Dar es Salaam